# Uelewa wa Fonetiki: Umuhimu wa Mashairi na Vitabu vya Alfabeti

## Kozi ya kitaalamu ya kujifunza kwa walimu wa elimu ya awali

*Uelewa wa mashairi kwa mtoto wa awali ni moja ya viashiria bora vya uwezo wao wa kusoma baadaye*
(Danielson, 2000 amenukuliwa na Redig, 2018)

Desemba 2023

Mshauri Education

Catherine Duffett
(Bsc(Hons), DipEd, Med(Teachlib), GradCertEd(LitEd)
Mwalimu wa Darasani kwa Mbinu ya Orton-Gillingham, Ngazi ya OGCE/OGA

info@mshauried.org

www.mshauried.org

## Kuhusu Mwandishi

Catherine Duffett ana uzoefu wa zaidi ya miaka ishirini kama mwalimu nchini Australia. Amefanya kazi Hobart, Darwin na Alice Springs katika shule za serikali na binafsi, zinazojumuisha wanafunzi kutoka tamaduni mbalimbali. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka kumi kama mhudumu wa maktaba kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, na kwa sasa anafanya kazi kama mhudumu wa maktaba wa shule ya msingi. Mwaka 2013 alitunukiwa tuzo ya "Mwalimu Bora wa Maktaba wa Tasmania wa Mwaka". Catherine pia amewahi kufundisha masomo ya Sayansi na Hisabati kwa wanafunzi wa sekondari. Yeye pia ni mtaalamu aliyebobea katika elimu ya usomaji.

Catherine ana shauku ya kutumia mbinu zenye ushahidi wa kisayansi zenye athari kubwa ili kuboresha fursa za kielimu kwa watoto, hasa wale wanaotoka katika mazingira magumu, na pia anafurahia kushiriki maarifa yake na wengine.
Catherine pia hufanya kazi kwa muda sehemu kama mshauri wa elimu kwa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) katika nchi zinazoendelea kwa kujitolea (pro bono), kusaidia kuboresha matokeo ya kielimu kwa watoto kutoka familia duni. Jina la biashara yake, **Mshauri Education**, alipewa na wenzake Watanzania, na "mshauri" ni neno la Kiswahili linalomaanisha **mshauri** au **mtaalamu.**

## Jinsi ya Kutumia Kozi Hii

Ingawa kozi hii inaweza kutumiwa na walimu binafsi kwa ajili ya mafunzo ya kitaalamu, inashauriwa kuwa, inapowezekana, walimu wafanye kazi kwa ushirikiano katika kupitia kozi hii, ili kuwezesha majadiliano ya kina na tafakari kuhusu utafiti uliotajwa. Ili kuwezesha hili, kozi imegawanywa katika sehemu mbalimbali zinazojumuisha maswali ya kujadili kwa ajili ya walimu kutafakari.

Mbinu ya *The Final Word* (Faddis, h.k) ni njia nzuri ya kujifunza kitaalamu, kwani huwezesha ushirikiano na tafakari ya kina juu ya maandiko. Mbinu hii hufanyika kwa namna ifuatayo:

1. Walimu hugawanywa katika makundi ya watu wanne, na kila mmoja hupewa jina A, B, C, au D. (Hii pia hufanya kazi kwa vikundi vya watu watatu).
2. Walimu husoma maandiko au sehemu ya maandiko, na huchagua kipande cha maandishi au nukuu iliyowagusa kisha huiandika kwenye kijikaratasi.
3. Mwalimu A huisoma kwa sauti nukuu au taarifa aliyochagua na anapewa dakika 3 kueleza kwa kundi lake sababu ya uchaguzi wake.
4. Walimu B, C, na D hupata dakika 1 kila mmoja kutoa maoni yao kuhusu nukuu ya Mwalimu A—hii inaweza kujumuisha mitazamo yao, kutoa ufafanuzi, au hata kuhoji mawazo ya Mwalimu A.
5. Mwalimu A hutoa muhtasari wa kile kilichojadiliwa na kueleza kama kuna kitu kimembadilisha mtazamo wake.

6. Mwalimu B naye huchagua nukuu yake na mchakato mzima hurudiwa kama ulivyokuwa kwa Mwalimu A, kwa walimu A, C, na D kujibu nukuu ya Mwalimu B.
7. Hatimaye, walimu C na D pia hupata nafasi ya kushiriki sehemu waliyochagua.
8. Vikundi tofauti hukutana kushirikiana mawazo yao.
9. Ili kuimarisha ujifunzaji, muda hutengwa kwa ajili ya walimu kutafakari juu ya yale waliyojifunza. pamoja na mshirika, waandike katika daftari maarifa mapya waliyopata au wapange hatua watakazochukua kwa kutumia maarifa hayo mapya.

**Shukrani**:

Asante kwa Fidelis Phene kwa kutafsiri programu hii kwenda lugha ya Kiswahili.

**Hati miliki:**

Leseni hii inaruhusu watumiaji tena kunakili na kusambaza nyenzo hii katika aina au njia yoyote ile, ikiwa haitabadilishwa, kwa matumizi yasiyo ya kibiashara pekee, na kwa sharti kwamba chanzo kitambuliwe kwa kutoa heshima kwa Mshaari Education.

**Maoni ya Wanaoshiriki (Feedback)**

Baada ya kumaliza kozi hii ya mafunzo ya kitaalamu, tafadhali chukua muda kujaza fomu ya mrejesho. Maoni yako ni muhimu kwa ajili ya kuboresha na kuunda programu nyingine bora zaidi za mafunzo ya kitaaluma.

(Scan QR code ifaayo hapa chini ili kufungua fomu sahihi ya maoni):

Maoni kutoka kwa viongozi wa shule

Maoni kutoka kwa walimu

# 1 Utangulizi

## Sehemu hii inajumuisha:

- Umuhimu wa watoto wadogo kujifunza kusoma.
- Sababu za kutumia vitabu vya alfabeti na vitabu vyenye mashairi na sauti zinazofanana kwa watoto wadogo.

Katika jamii inayotegemea maandishi, kujifunza kusoma ni moja ya mambo muhimu yanayoathiri maisha ya mtoto, kwani kupitia kusoma ndipo wanajamii hupata maarifa kwa kiwango kikubwa. (Cox na wenzake, 2019). Uwezo wa mtoto wa kusoma huwa kiashiria muhimu cha mafanikio yao kielimu na huathiri kiwango cha ushiriki wao katika jamii hiyo na uwezo wa kuishi maisha yenye maana.

Walimu wa elimu ya awali wana jukumu kubwa katika kuendeleza ujuzi wa watoto wa kusoma mapema ili kuwasaidia kuwa wasomaji. Kusoma kwa pamoja, ambapo mwalimu husoma kwa sauti na kuwahusisha watoto katika majadiliano kuhusu yaliyosomwa, ni njia ya kuvutia watoto na yenye ufanisi mkubwa wa kuboresha ujuzi wa kusoma kwa watoto.

Kozi hii inazingatia utafiti unaotegemea ushahidi ambao unaunga mkono usomaji wa mara kwa mara wa vitabu vya alfabeti na vile vyenye mashairi na maneno yenye sauti zinazofanana.

## Umuhimu wa mashairi, sauti zinazofanana na vitabu vya alfabeti

Uelewa wa mtoto wa elimu ya awali kuhusu mashairi (ikiwa ni pamoja na mashairi ya utotoni) ni kati ya viashiria bora vya uwezo wao wa kusoma baadaye (Danielson, 2000 alinukuliwa na Redig, 2018).

Mashairi husaidia kukuza ujuzi wa awali wa kusoma kwa watoto. Mbali na kuburudisha, vitabu vya mashairi (ikiwemo mashairi ya utotoni) huwasaidia watoto kujifunza kuhusu muundo wa simulizi, kukuza ujuzi wa kijamii na kuelewa sentensi na misemo rahisi (Sayakhan & Bradley 2019).

Mashairi pia yana nafasi kubwa katika kukuza uelewa wa sauti za lugha (yaani, uwezo wa kuchezea na kubadili sauti ndani ya maneno) ambao ni ujuzi muhimu kwa ajili ya kutambua maneno kwa ufanisi.

Vitabu vya alfabeti pia ni nyenzo muhimu kwani husaidia watoto kujifunza majina ya herufi na sauti zinazowakilishwa na herufi hizo.

Utafiti uliojadiliwa katika kozi hii unahusiana na lugha yoyote iliyoandikwa.

### Tafakari na Jadili

1. Mara ngapi unatumia mashairi na maneno yenye sauti zinazofanana katika programu yako ya elimu ya awali?

2. Ni hadithi zipi zenye mashairi (ikiwemo mashairi ya utotoni) unazotumia katika programu yako?
3. Uelewa wako wa sasa ni upi kuhusu jinsi mashairi, maneno yenye sauti zinazofanana na kujifunza alfabeti vinavyosaidia kukuza ujuzi wa awali wa kusoma kwa watoto?

## 2 Awamu za Awali za Kujifunza Kusoma

Sehemu hii inajumuisha:
- Kutambua awamu nne za usomaji
- Kujadili awamu mbili za usomaji zinazohusiana na elimu ya awali ya watoto

### Awamu za Ukuaji wa Kusoma

Linnea Ehri alitambua kuwa wasomaji wote hupitia awamu nne za kujifunza kusoma wanapokuwa mahiri zaidi katika usomaji (Cook Moats, 2020). Wakati wa kupanga shughuli za ujifunzaji ili kuboresha ujuzi wa awali wa kusoma kwa watoto (ikiwemo usomaji wa pamoja), ni muhimu kuzingatia awamu hizi za maendeleo ya usomaji wakati wa kubuni kazi zinazofaa kimaendeleo.

### Awamu ya Awali Kabla ya Kutambua Herufi (Pre-Alphabetic Phase) (Awamu ya kwanza ya Ehri)

Watoto hupitia awamu hii hadi wanapofikia umri wa takribani miaka 4. Vipengele vya kawaida vya awamu hii ni:

**Uelewa wa Sauti za Herufi:**
Katika awamu hii, watoto kwa kawaida hawana uelewa wa kutosha wa sauti na herufi zinazowakilisha ili waweze kukumbuka maneno kwa kudumu. Badala yake, hutegemea ishara za kuona au kujifunza kwa kukariri kusaidia kuhifadhi maneno katika kumbukumbu zao. (Cook Moats, 2020). Kwa mfano, Kilpatrick (2016) anaeleza kuwa kwa neno **look**, mtoto anaweza kulikumbuka kwa kuangalia herufi mbili 'o' zinazofanana na macho mawili, njia ambayo si bora katika kujifunza maneno mapya kwa sababu humfanya mtoto akumbuke maneno kwa sura badala ya ujuzi wa sauti za herufi.

**Dhana ya Uchapaji (Concepts of Print):**
Watoto katika awamu hii huanza kuelewa kuwa kitabu husomwa kuanzia kushoto kwenda kulia, kutoka juu kwenda chini, na maandiko hutenganishwa kwa nafasi, n.k. Maarifa haya yanaitwa **dhana ya uchapaji** (Cook Moats, 2020).

### Awamu ya Herufi Nusu (Partial Alphabetic Phase) (Awamu ya pili ya Ehri)

Awamu hii hujitokeza mtoto anapoanza kutumia maarifa ya sauti za herufi ili kuhifadhi maneno katika kumbukumbu. Kwa kawaida, wanaweza kufananisha sauti moja au mbili za mwanzo na herufi ya mwanzo ya neno, japokuwa wanaweza kuwa na uwezo mdogo sana wa kufananisha sauti nyingine na herufi zake. Kilpatrick (2016) anatoa mfano wa neno stand. Watoto katika awamu hii wanaweza kuwa wamefananisha herufi ya kwanza na ya mwisho ya neno na hivyo kulikumbuka kwa urahisi baadaye. Hata hivyo, wakiona neno linalofanana kama sand, wanaweza kuchanganya na stand kwa sababu wamehifadhi sehemu tu ya neno.

### Tafakari na Jadili

Kutafakari juu ya awamu ya awali na ya herufi nusu: Ni uzoefu gani wa ujifunzaji unaotumika kwa sasa kusaidia kukuza ujuzi wa awali wa kusoma kwa watoto?

# 3 . Ujuzi Unaohitajika kwa Ajili ya Kusoma Kwa Ufanisi

**Sehemu hii inahusisha**:
- Muhtasari wa Kamba ya Usomaji ya Scarborough
- Jinsi vina (rhymes) vinavyoweza kusaidia kufundisha ujuzi fulani wa kusoma na kuandika

## Kamba ya Usomaji ya Scarborough

Utafiti umeonyesha kuwa uwezo wa kufasiri maneno (decode) na kuelewa lugha unategemea vipengele kadhaa, ambavyo vinaonyeshwa kupitia Kamba ya Usomaji ya Scarborough (Mchoro wa 1) *.* Mfano huu ni chombo chenye nguvu kwa ajili ya kufundishia darasani na pia kubaini matatizo yanayowakumba wasomaji wanaojikuta wakihangaika kujifunza kusoma (Lewis Hennessy, 2021).


Mfano huu unaonyesha kwamba:

- kuna vipengele viwili vikuu vya usomaji wa ufanisi: utambuzi wa maneno (word recognition) na uelewa wa lugha (language comprehension)
- uelewa mzuri wa maneno na lugha hutegemea ujuzi mbalimbali, na kuwa mahiri katika kila kipengele ni muhimu ili mtu awe msomaji stadi (Lewis Hennessy, 2021).

Kozi hii inajikita zaidi kwenye uelewa wa sauti (phonological awareness), ambao ni ujuzi muhimu kwa ajili ya kutambua maneno kwa ufanisi.

## Tafakari na Jadili

1. Unafahamu kwa kiwango gani kuhusu kila kipengele cha Kamba ya Usomaji ya Scarborough?
2. Unawezaje kutumia mfano huu kusaidia kupanga kazi za ujifunzaji darasani?





**Mchoro wa 1: Kamba ya Kusoma ya Scarborough (Scarborough, 2001, alinukuliwa na Lewis Hennessy, 2021)**

**Translation of Scarborough's Reading Rope**

Utambuzi wa Maneno
- **Uelewa wa sauti (phonological awareness)** — silabi, fonimu n.k.
- **Ufumbuzi wa maneno kwa kutumia herufi-sauti (decoding)** — kanuni za kisauti na herufi
- **Utambuzi wa maneno kwa kuona (sight recognition)** — kutambua maneno yanayojirudia

**Uelewa wa Lugha**
- **Maarifa ya awali (background knowledge)** — ukweli, dhana, n.k.
- **Msamiati (vocabulary)** — upana na kina cha maneno
- **Miundo ya lugha (language structures)** — sarufi, sentensi
- - **Uwezo wa hoja (verbal reasoning)** — hitimisho, mafumbo, n.k.
- **Maarifa ya kusoma na kuandika (literacy knowledge)** — dhana za uchapaji, n.k.

## 4 Uelewa wa Fonolojia na Kanuni ya Alfabeti




**Mchoro wa 2: Ngazi 5 za Uelewa wa Fonolojia (Kutoka: *Basics: Phonological and Phonemic Awareness: Reading Rockets, 2023)***

Kielelezo kinaonyesha hatua tano za uelewa wa fonolojia kuanzia shughuli rahisi hadi ngumu zaidi:

1. Vina na Aliteresheni
2. Ugawanyaji wa Sentensi
3. Silabi – kugawa na kuunganisha
4. Sauti za mwanzo na vina – kuunganisha na kugawa
5. Uelewa wa Fonetiki – kuchanganya sauti, kugawa maneno kuwa sauti, kufuta au kubadili sauti katika maneno yanayozungumzwa.

**Sehemu hii inahusisha**:

Kipengele hiki kinajumuisha
• ufafanuzi wa uelewa wa kifonolojia
• jinsi uelewa wa kifonolojia unavyokua na athari zake katika ufundishaji na ujifunzaji

### Uelewa wa Fonolojia ni nini?

Uelewa wa fonolojia ni utambuzi kwamba sauti katika lugha inayozungumzwa zinaweza kubadilishwa (Dougherty Stahl, 2020). Kama Kamba ya Usomaji ya Scarborough inavyoonyesha, uelewa huu ni nyenzo muhimu ya kusaidia utambuzi wa maneno.

Uelewa wa fonolojia umegawanyika katika:

- uelewa wa sauti kwa ujumla (phonological sensitivity)
- uelewa wa sauti mahususi (phonemic awareness)

## Uelewa wa Sauti kwa Ujumla (Phonological Sensitivity)

Unahusu utambuzi wa vitengo vikubwa vya sauti kama:
**Vina na aliteresheni** – uwezo wa kutambua kama maandishi yana vina au alama za mwanzo zinazojirudia.
**Ugawanyaji wa sentensi** – uwezo wa kutambua maneno ya kipekee ndani ya sentensi.

*Silabi*
Ni uwezo wa kutenganisha silabi kwenye maneno. Mfano, katika neno *cucumber*, mtoto anaweza kupiga makofi kutambua kuwa kuna silabi tatu: *cu-cum-ber.*
Pia, mtoto anaweza kupewa silabi *blan* na *ket* na kutakiwa kuziunganisha kutengeneza neno *blanke*t (Kilpatrick, 2016).

*Sauti za mwanzo na vina (Onset and Rime)* - *Onset* ni konsonanti inayoanza kabla ya vokali kwenye silabi. Mfano, katika neno *sat*, sauti ya mwanzo ni *s*.
- *Rime* (*si rhyme*) ni sehemu ya neno yenye vokali na konsonanti zinazofuata. Katika *sat***,** rime ni *at* (Kilpatrick, 2016).

*Uelewa wa Fonetiki (Phonemic Awareness)* **-** Ni uwezo wa **kutambua na kubadilisha sauti za mtu mmoja mmoja** (fonimu) ndani ya maneno yanayozungumzwa (Kilpatrick, 2016).

## Fonimu ni nini?

Neno *phoneme* linatokana na neno la Kigiriki *phonos,* lenye maana ya *sauti* au *mlio*. Fonimu ni kipande kidogo kabisa cha sauti katika maneno yanayozungumzwa.
Mfano: neno *pat* lina fonimu tatu: */p/ /a/ /t/* (alama za mabano zinaonyesha sauti, si herufi).
Neno ***pluck*** lina herufi 5 lakini lina fonimu 4: */p/ /l/ /u/ /ck/.*

## Ukuaji wa Uelewa wa Fonolojia

Katika hatua ya awali kabla ya kufahamu alfabeti, watoto huanza kukuza uelewa wa awali wa fonolojia. Kwa kawaida, ifikapo miaka minne, watoto wanaweza:
- Kutambua vina na aliteresheni (maneno yanayorudiarudia sauti)
- Kutofautisha silabi ndani ya maneno

Watoto wa miaka mitano wanapaswa kuweza kuunganisha silabi kutengeneza maneno mapya (Cook Moats, 2020).

## Wanaojifunza Kiingereza

Utafiti huu unaweza kutumika kujifunza lugha yoyote. Lengo likiwa ni kuweza kuelewa Kiingereza na lugha nyingine kwa ufanisi, basi watoto wanapaswa kukuza ujuzi wa uelewa wa fonolojia katika lugha zote mbili kwa wakati mmoja (Stewart, 2004).

## Matumizi ya Utafiti katika Kufundisha

Watoto wanaposhiriki kwenye michezo ya maneno kama vina na aliteresheni, wanajifunza kuzingatia sauti badala ya maana ya maneno (Kilpatrick, 2016). Mwalimu anaweza kutumia beti ya watoto kama:

*Jack and Jill went up the hill to fetch a pail of water,*
*Jack fell down and broke his crown,*
*And Jill came tumbling after.*

Watoto wanaweza kuulizwa:

- Ni maneno gani yana vina na *Jack?*
- Ni maneno yapi yanaanza kwa sauti sawa na *Jack*?

Maswali haya husaidia kukuza uelewa wa sauti na vina.

## Nafasi ya Vitabu katika Kukuza Uelewa wa Fonolojia

Vitabu vyenye vina na mashairi (kama nursery rhymes) ni muhimu sana. Kwa mujibu wa tafiti, uelewa wa mashairi huashiria uwezo mzuri wa baadaye wa kusoma (Danielson, 2001).

Vitabu hivi:

- Huchochea uelewa wa fonolojia
- Husaidia watoto kuelewa miundo ya hadithi
- Hukuza stadi za kijamii
- Hufundisha misemo rahisi na sentensi fupi (Sayakhan & Bradley, 2019).

## Wanaojifunza Kiingereza kama Lugha ya Ziada

Kwa watoto wanaojifunza Kiingereza kama lugha ya pili, Sayakhan na Bradley (2019) wanaeleza kuwa usomaji na uimbaji wa mashairi ya Kiingereza kwa kurudia rudia huwasaidia kukuza uelewa wa lugha ya mazungumzo. Watoto wanajifunza kwa kusikia vina vya Kiingereza na kuvikariri kwa sauti.

## Kanuni ya Alfabeti

*Kuvunja maneno (Decoding)* ni mchakato wa kubadilisha maneno yaliyoandikwa kuwa maneno yanayozungumzwa.
*Kanuni ya alfabeti* ni uelewa kuwa kila herufi inawakilisha sauti au fonimu mahususi. Hili ni muhimu ili kufanikisha kuvunja maneno yaliyopo kwenye maandishi. Mfano: Alfabeti ya Kiingereza ina herufi 26 lakini ina fonimu zaidi ya 44 (Arthur na Hertzberg, 2018).

Kwa mujibu wa Dougherty Stahl na wenzake (2020), uzoefu wa kujifunza kwa watoto walio katika hatua ya awali kabla ya kuelewa alfabeti unapaswa kujumuisha shughuli za kukuza maarifa ya:
- Majina ya herufi
- Sauti za herufi
- Namna ya kuziandika

Vitabu vya alfabeti vinafaa sana kwa kazi hii. Stein (2015) anapendekeza matumizi ya *mbinu ya Four S* (S nne) kusoma vitabu vya alfabeti kwa sauti kwa watoto ili kuongeza ufanisi wa kujifunza.

**Mbinu ya S Nne (Four S's Strategy):**
Mbinu hii hutumia hatua zifuatazo:
1. ***Show (Onyesha)***: Mwalimu anaonyesha herufi.
2. ***Say (Sema):*** Mwalimu anasema jina la herufi.
3. ***Sound (Toa Sauti)***: Mwalimu anasema sauti ya herufi hiyo. Mfano: /a/ kama kwenye "apple".
4. ***Stress (Tilia Mkazo)***: Mwalimu anasisitiza sauti hiyo. Mfano: *a-a-a-apple au mmmm – mouse.*

## Tafakari na Jadili

1. Kwa nini kukuza uelewa wa kifonolojia kwa watoto kunapaswa kuwa sehemu muhimu ya programu za elimu ya awali ya mtoto?
2. Kusoma mashairi au vina kwa watoto kunawezaje kuwasaidia kukuza ujuzi wao wa kifonolojia?
3. Panga uzoefu wa kujifunza ujao unaojumuisha mashairi na nyimbo.
4. Ni uzoefu gani mwingine unaweza kuujumuisha ili kuendeleza zaidi uelewa wa kifonolojia kwa watoto?
5. Panga uzoefu wa kujifunza ambapo mkakati wa "Four S's" utatumika pamoja na kitabu cha alfabeti.

## Hitimisho

Vitabu vya alfabeti na vile vyenye vina na aliteresheni (maneno yanayorudiarudia sauti) ni njia bora na yenye mvuto kwa watoto ili:

- Kuelewa kanuni ya alfabeti
- Kukuza uelewa wao wa fonolojia

Ujuzi huu wa awali wa kusoma ni muhimu sana kwa mafanikio ya baadaye ya mtoto katika kusoma Kiingereza au lugha yoyote inayotumia alfabeti.

# Fasili ya Maneno Muhimu (Glossary)

**Aliteresheni:**
Aliteresheni ni mbinu ya kifasihi inayotumika katika uandishi na ushairi ambapo mfululizo wa maneno katika sentensi au kifungu huanza na sauti ile ile ya konsonanti. Kwa mfano, "Peter Piper picked a peck of pickled peppers" ni mfano maarufu wa aliteresheni.

**Kanuni ya Alfabeti (Alphabetic Principle):**
Kanuni ya alfabeti inahusiana na uelewa kwamba herufi katika alfabeti zinawakilisha sauti mahususi za usemaji (fonimu). Kwa maneno mengine, ni uelewa kwamba herufi katika maandishi zinahusiana na sauti maalum katika lugha ya mazungumzo. Maarifa haya ni muhimu sana katika kujifunza kusoma na kuandika kwa kutumia maandishi ya alfabeti.

**Kuvunja Maneno (Decoding):**
Kuvunja maneno ni mchakato wa kubadilisha maandishi kuwa lugha ya mazungumzo. Katika muktadha wa usomaji, hii inahusisha maarifa ya uhusiano kati ya herufi na sauti (foniksi) na kanuni ya alfabeti ili kusoma maneno na kuelewa maana yake.

**Uelewa wa Lugha (Language Comprehension):**
Uelewa wa lugha ni uwezo wa kuelewa na kupata maana kutoka kwa lugha ya mazungumzo au maandishi. Hii inahusisha kutafsiri maneno, sentensi na aya, pamoja na kuelewa maana ya ujumla wa mawasiliano.

**Usomaji wa Pamoja (Shared reading):**
Usomaji wa pamoja ni shughuli ya kusoma kwa kushirikiana na kwa njia ya mwingiliano ambayo inahusisha watoto na mwalimu wakisoma maandiko pamoja. Wakati wa usomaji wa pamoja, mwalimu husoma maandishi kwa sauti, kama vile kitabu cha picha au hadithi fupi, huku akihamasisha ushiriki hai, majadiliano, na mwingiliano kutoka kwa watoto.

**Silabi (Syllable):**
Silabi ni kitengo cha lugha ya mazungumzo ambacho kawaida hujumuisha sauti moja ya irabu (au sauti ya irabu pamoja na konsonanti zinazoambatana nayo). Silabi huunda msingi wa maneno na kusaidia katika kubainisha matamshi yao. Kwa mfano, neno "but-ter-fly" lina silabi tatu.

**Marejeleo:**

Arthur, L., & Hertzberg, M. (2019). **Kanuni ya alfabeti katika elimu ya awali ya kusoma na kuandika.** Katika **The alphabetic principle and beyond: surveying the landscape** (uk. 81–101). Primary English Teaching Association Australia.

Cook Moats, L. (2020). **Kutoka sauti hadi maandishi: misingi ya lugha kwa walimu**. (Toleo la 3). Brookes Publishing Co.

Cox, R., Freez, S., & Beveridge, L. (2019). **Usomaji: shughuli muhimu katika jamii yetu.** Katika **The alphabetic principle and beyond: surveying the landscape*** (uk. 2–11). Primary English Teaching Association Australia.

Dougherty Stahl, K. A., Flanigan, K., & Mckenna, M. C. (2020). **Tathmini ya Mafunzo ya Usomaji** (Toleo la 4). Guilford Press.

Faddis, T. (bila tarehe). **Kukuza Mafunzo Endelevu ya Kitaaluma kwa Kutumia Maandishi na Itifaki za Majadiliano | International Literacy Association**. Imepatikana Disemba 7, 2023 kutoka: https://www.literacyworldwide.org/get-resources/instructional-practices/promoting-ongoing-professional-learning-using-text-and-discussion-protocols?Site=ILA

Kilpatrick, D. A. (2016). **Kujiandaa kwa mafanikio ya usomaji: Mpango wa hatua kwa hatua wa kukuza uelewa wa fonimu na utambuzi wa maneno kwa ufasaha**. Casey & Kirsch Publishers.

Lewis Hennessy, N. (2021). **Muundo wa uelewa wa usomaji: kusaidia wanafunzi kupata maana kutoka kwenye maandiko.** Paul H. Brookes Publishing Co.

Redig, J. (2018). **Je, Mfiduo wa Kila Siku kwa Mashairi ya Watoto Unaboresha Uelewa wa Fonolojia kwa Wanafunzi?** [Tasnifu ya Uzamili]. https://nwcommons.nwciowa.edu/cgi/viewcontent.cgi?article=1095&context=education_masters

Sayakhan, N. I., & Bradley, D. H. (2019). **Mashairi ya Watoto kama Njia ya Kufundisha Kiingereza kama Lugha ya Kigeni.* *Jarida la Chuo Kikuu cha Raparin, 6**(1), 44–55. https://doi.org/10.26750/vol(6).no(1).paper4